

JINA LA MTAHINIWA		NAMBARI YA MTAHINIWA	
JINA LA SHULE YAKO		NAMBARI YA SHULE	
SAHIHI YA MTAHINIWA		TAREHE	



003-2025

Karatasi ya 2
Muda: Saa 1 Dakika 45

JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

GREDI YA 9

JESMA
003

- KISWAHILI-

(Insha na Utangulizi wa Fasihi)

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Andika **jina** lako na **nambari** yako ya mtihani kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
2. Andika **jina** na **nambari** ya **shule** yako kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
4. Andika **tarehe** ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B.
6. Jibu maswali yote.
7. Andika majibu yote kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

SEHEMU	A	B			
	Zoezi I Swali:1	Zoezi II Swali: 2	Zoezi III Swali:3	Zoezi IV Swali:4	Zoezi V Swali:5
Alama ya upeo	15	10	10	10	5
Alama ya mtahiniwa					

Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote
za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Geuza ukurasa

SEHEMU A: (Alama 15)

ZOEZI I - INSHA.

Maagizo:

- i) Inapendekezwa uchukue muda wa dakika 40 katika zoezi hili.
- ii) Andika insha yenye maneno kati ya 300 - 350 katika nafasi uliyoachiwa.

Anza hivi:

Ilikuwa siku ya Ijumaa nilipoamka nikiwa nimejawa na furaha na buraha

.....

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are approximately 20 lines visible. The paper appears slightly aged or off-white. There is no handwriting or other markings on the page.

ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

Mekatilili Wa Menza ni mwanamke wa nchini Kenya aliyewaongoza Wagiriana dhidi ya utawala wa kikoloni mwaka wa 1913 hadi 1914. Wagiriana ni watu wa kabila moja katika kundi la makabila tisa (Mijikenda) ambao hukaa pwani ya Kenya; walikuwa na maskani takatifu sehemu ziiwazo Kaya, ambazo zilipatikana katika maeneo ya misitu, mojawapo ambayo iliharibiwa kwa kulipuliwa na utawala wa kikoloni wa Uingereza mwaka wa 1914. Hii ilikuwa Kaya Fungo.

Mekatilili alizaliwa katika miaka ya 1860 huko Bamba katika kaunti ya Kilifi. Alikuwa binti pekee katika familia ya watoto watano. Alionekana simba kwa ujasiri aliokuwa nao. Kaka yake mmoja alitekwa nyara na Waarabu wafanyabiashara ya utumwa na hakuwahi kuonekana tena. Jambo hili lilimkasirisha sana akawa na hasira kama za mkizi. Walipigana kule msituni na barabarani walipokutana na wakoloni hao.

Mekatilili alipinga utawala wa kikoloni kutokana na sababu za kiuchumi na kijamii. Hakutaka Wagiriana kuajiriwa na serikali ya kikoloni maana alitaka wabaki nyumbani mwao waifae jamii. Pia aliona kuwa mila na desturi za Mwingereza zilikuwa zikiingilia mila na desturi za Wagiriana, jambo lililomhuzunisha. Awali alikuwa ametabiri ujio wa Waingereza ambao aliwataja kama watu wenye nywele sawia na makonge, waliozunguka kupitia vyombo vya angani na majini.

Mekatilili Wa Menza anasifika sana kwa kuwashawishi Wagiriana kukaidi utawala wa ukoloni ambao ulikuwa unawafanya watu wake kuwa watumwa na kutozwa ushuru ghali. Awali alikuwa ametabiri ujio wa Waingereza ambao aliwataja kama watu wenye nywele sawia na makonge, waliozunguka kupitia vyombo vya angani na majini. Mekatilili alikamatwa na kufungwa katika gereza moja la Kismayu. Mekatilili Wa Menza alivumilia kama mtumwa kweli. Alipiga moyo konde na kuendelea kupigana.

Asubuhi moja mwendo wa saa tano, Mekatilili alitiwa mbaroni na Waingereza na kupelekwa uhamishoni Mumias katika Mkoa wa Magharibi wa Kenya. Kulingana na rekodi za ukoloni wa Uingereza, alirejea katika eneo lake la uraia miaka mitano baadaye ambapo aliendelea kupinga kulazimishwa kwa sera na amri za kikoloni. Alifariki mwaka wa 1924 akazikwa Bungale, katika Jimbo la Magarini.

1. Hurafa ni hadithi ambayo wahusika ni wanyama. Bainisha kipera au aina ya hadithi hii uliyoisoma. (Alama 1)

2. Mtu anayezungumziwa hapa ni mfano wa _____ ambaye pia huitwa shujaa. (Alama 1)
3. Bainisha aina **mbili** za mbinu ambazo zimejitokeza kwenye hadithi hii. (Alama 2)
 - a) _____
 - b) _____

4. Eleza sifa **tatu** za aina ya hadithi hii uliyoisoma. (Alama 3)
- a) _____
- b) _____
- c) _____
5. Taja aina **mbili** za mandhari ambazo zimejitokeza katika kisa hiki (Alama 2)
- a) _____
- b) _____
6. Ni funzo gani unalopata kutoka kwa 'Mekatilili'. (Alama 1)
- _____

ZOEZI III : NOVELA (Alama 10)

Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali.

Dereva wa garimoshi aliitia injini moto saa nane u nusu juu ya alama. Kule kwenye dirisha Herina aliona chombo hiki kikianza safari polepole na hatimaye kukaza mwendo. Kwa hakika alikipenda chombo chenyewe. Hiki hakikuwa kama yale magari moshi ya kawaida ambayo yalienda kwa mwendo wa konokono. Herina alikuwa ameambiwa kwamba hiki kilikuwa na mbio za swara. Walitarajia kuwasili katika mji wa Matarajio baada ya saa tano. Hili lilimtuliza Herina kidogo. Aliona safari hii kuwa fupi kuliko ile ya basi ambayo alisikia inachukua saa saba au nane.

Sauti ya mhudumu ilisikika tena kupitia kwenye kifaa fulani cha kidijitali. Iliwatangazia kwamba chombo kilikuwa kimeng'oa nanga. Iliwaeleza kuhusu urefu wa safari yao. Iliwatangazia wanakoweza kupata vyumba vya kwenda haja. Iliwatangazia pia saa ambayo walitarajiwa kufika walikokuwa wanaenda. Sauti ya mhudumu huyo ilimtia Herina matumaini zaidi. Alikuwa na hamu ya kufika kwenye Mji wa Matarajio. Alikuwa amesoma mtandaoni kuhusu mji huu. Hivi majuzi alikuwa amesoma kwenye mtandao kuhusu maliasili inayopatikana katika mji huu. Mji huu ulizungukwa na bahari yenye maji ya chumvi na wanyama mbalimbali wa majini. Ulibarikiwa kuwa na fuo zenye mchanga unaovutia watalii, minazi mirefu ya kuvutia na mikoroshu. Alitumaini kuwa angepata muda wa kujionea haya yote, pengine mwishoni mwa Juma.

Garimoshi lilitafuna masafa kama mja mwenye njaa. Kutanabahi, walikuwa wamelipita daraja la Mto wa Tumaini. Huu ndio uliokuwa mto mkubwa zaidi katika eneo hili. Maji mengi nchini, hata yale waliyokuwa wakitumia akina shangazi, yalitoka humu. Lililomvutia Herina zaidi kuhusu mto huu ni kwamba binadamu hakuwa ameuingilia. Hakuwaona watu wakifulia nguo na kuogea kwenye kingo za mto huo kama ilivyokuwa desturi ya baadhi ya watu huko alikotoka.

"Haikosi haya yana wavuvi ambao wanajitayarishia shughuli za uvuvi," Herina alijisemea.

Herina aliutazama mto huo hadi ulipopotea kwenye upeo wa macho yake. Aliufungua mkanda wa usalama na kusimama ili angalau apate kujinyoosha. Herina alikuwa amejifunza kutoketi kwa muda mrefu sana. Hata alipokuwa akidurusu shuleni na nyumbani, alizoea kuinuka baada ya saa moja au mbili. Hapo, angetembea kidogo na kuiruhusu damu kutembea miguuni.

1. Herina ni msichana mwenye hekima. Eleza sifa nyingine mbili za Herina. (Alama 2)
 - a) _____
 - b) _____
2. Taja mbinu mbili zilizotumika katika sehemu ya novela uliyoisoma (Alama 2)
 - a) _____
 - b) _____
3. Novela ni riwaya fupi. Taja sifa tatu za novela. (Alama 3)
 - a) _____
 - b) _____
 - c) _____
4. Ploti ni mtiririko wa matukio katika kazi ya fasihi pia huitwa; (Alama 1)

5. Eleza funzo unalopata kutoka kwa Herina. (Alama 1)

6. Taja maudhui yanayojitokeza katika makala haya ya novela. (Alama 1)

ZOEZILA IV: TAMTHILIA (Alama 10)

Sehemu ya 3

Onyesho la 2

Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.

(Ni saa moja na nusu Karimi anapofika nyumbani akitoka shuleni. Anaingia nyumbani na kuwakuta wameketi kimya huku wamenyamaza ji!)

Baba : Kitu gani kinachokufanya kuchelewa kurudi nyumbani mapema kila siku?

Karimi : Kuna mchezo shuleni na tunalazimishwa kushiriki

Baba : Kwani michezo shuleni inachezwa hadi saa tatu usiku?

Karimi : Baba, walimu hutuambia ni vyema kushiriki michezo pamoja na masomo vilevile

Baba : Walimu wanafanya wajibu wao, lakini mbona michezo mpaka saa hizi?

Mama : Pengine alichelewa njiani akirudi. Unajua vijana?

Baba : *(akimkatiza mama)* Kwa hivyo?

Mama : Nakumbuka, shuleni kuna sheria ambazo ni lazima zifuatwe. Walimu hawawezi kuwafungia wanafunzi uwanjani hadi sasa hizi?

Baba : Kwa hivyo unasema ni sawa kwa Karimi kuja nyumbani akiwa amechelewa?

Mama : La hasha, Pengine mwenyewe atueleze alikochelewa

Baba : Yaani mtoto akikosa adabu asifunzwe?

- Mama** : Baba Karimi, hujanielewa. Ninasema tumpe nafasi naye ajieleze. Akisha jieleza uamuzi utakuwa ni wetu sasa. Kama amekosea, tumwadhibu inavyostahiki.
- Baba** : Haya Karimi, mbona unajikunyata hivyo?
- Karimi** : Baba tuliporuhusiwa kwenda nyumbani nilipitia kwa kina Rukia. (*Kwa sauti ya chini*) Baba, kina Rukia wamenunua mbwa wa kizungu. Ana manyoya mengi hadi usoni. Nilichelewa kwao nikicheza naye. Baba, unaweza kuninunulia mbwa kama wa kina Rukia?
- Baba** : (*Akimvuta kwake*) Karimi, ulifanya makosa kupitia kwa rafiki yako jioni. Kutembea peke yako usiku kuna hatari nyingi. Ni kweli rafiki yako ana mbwa wa kizungu, na wewe huna. Hata nawe una baiskeli ambayo hana.
- Mama** : (*Akimkatiza baba*) Karimi, anachokuambia baba yako ni kweli. Juzi tu uliletewa mpira na shangazi yako. Mwanangu, duniani humu sisi sote hatuwezi kuwa sawa. Utakosa hiki na mwenzako atapata kingine. Huwezi kuwa na kila kitu.
- Karimi** : (*Akitabasamu*) Ni kweli sisi sote si sawa. Ninashukuru kuwa na wazazi wanaonipenda. Baba, mama, sitachelewa tena kufika nyumbani.
- Baba** : Haya basi, nenda kamsaidie ndugu yako kuandaa meza tupate chajio hata sisi tumechelewa kula.

(Karimi anatoka upesi. Mama na baba wanabaki sebuleni wakizungumza)

1. Taja wahusika **wawili** wakuu wa mazungumzo haya. (Alama 2)
 a) _____
 b) _____
2. Kwa mujibu wa mazungumzo haya, taja sifa **mbili** za Karimi. (Alama 2)
 a) _____
 b) _____
3. Unadhani ni kwa nini baba Karimi alikuwa amekasirika? (Alama 1)

4. Taja mandhari ya onyesho hili. (Alama 1)

5. Taja mbinu **mbili** za lugha ambazo zimejitokeza katika tamthilia hii. (Alama 2)
 a) _____
 b) _____
6. Dhamira tunayoipata kutokana na tamthilia hii ni; (Alama 2)

ZOEZI V: USHAIRI (Alama 5)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Kuna mingi na shambani, mimea ile mizuri
Ina vingi vitamini, tunaonea fahari
Ikifika na tumboni, twapata nzuri Habari
Lishe kwetu ni muhimu, vyakula bora tuleni

Sisahau protini, mili ipate nawiri
Sote tuyale maini, afia iwe vizuri
Si enzi za kikoloni, mili yetu tuvinjari
Lishe kwetu ni muhimu, vyakula bora tuleni

Tule kwa wingi mahindi, mili ipate ushindi
Tusiwe kama hindi, michezo tuwe vikundi
Hata kama ni Atandi, isitunate na gundi
Lishe kwetu ni muhimu, vyakula bora tuleni

Tomoko pia mapera, sitazame kwayo hasira
Tusiache vipera, matunda haya imara
Tule mimea ya bara, afya iwe barabara
Lishe kwetu ni muhimu, vyakula bora tuleni

Zaidi tupige dua, kudura za Manani
Ndiye Mungu wetu pia, kwa kila jambo jamani
Huleta nayo mvua, mavuno tele ghalani
Lishe kwetu ni muhimu, vyakula bora tuleni

1. Andika aina mbili za vyakula zinazotajwa na mtunzi. (Alama 2)
a) _____
b) _____
2. Ujumbe maalum wa shairi hili ni; (Alama 1)

3. Tambua vina vya ubeti wa pili kama vinavyojitokeza katika shairi hili. (Alama 1)

4. Mtunzi ana ujumbe gani kwetu kuhusu Maulana? (Alama 1)
